# Curriculum design
# Kiswahili grade

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Shuleni** | Sauti na majina ya herufi za Kiswahili (*Vipindi 8*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutamka sauti nne za herufi moja ili kuimarisha mazungumzo<br>b) kutambua sauti za herufi moja zilizofunzwa katika kujenga stadi ya kusikiliza<br>c) kutambua majina ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kujenga stadi ya kusikiliza<br>d) kusoma herufi za sauti moja katika kujenga stadi ya kusoma<br>e) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa katika kujenga stadi ya kusoma<br>f) kusoma vifungu vilivyo na maneno yaliyo na sauti lengwa katika kujenga stadi ya kusoma<br>g) kuandika herufi zinazowakilishwa na sauti lengwa katika kujenga stadi ya kuandika<br>h) kuchangamkia kutumia maneno yanayojumuisha sauti zilizofunzwa katika mawasiliano ya kila siku. | • Mwanafunzi aweza kutambua sauti /g/, /d/, /j/, na /r/ katika maneno.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu akitamka sauti lengwa, kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili na kama darasa.<br>• Mwanafunzi atambue sauti alizosoma katika maneno.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia teknolojia (papaya) kusikiliza matamshi ya sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi.<br>• Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno.<br>• Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi au kwa kuyagawa maneno marefu katika sehemu fupi fupi.<br>• Mwanafunzi aandike herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni.<br>• Mwanafunzi aweza kufinyanga maumbo ya herufi. | 1) Je, ni sauti zipi unazojua kutamka?<br>2) Unajua kusoma herufi na maneno gani?<br>3) Unajua kuandika herufi na maneno gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Wanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta na kipasa sauti kusikiliza na kusoma hadithi.<br>• Mwanafunzi anakili herufi na maneno yanayotokana na sauti alizofunzwa.<br>• Mwanafunzi aandike maumbo ya herufi na maneno yaliyo na herufi za sauti alizofunzwa.<br>• Mwanafunzi asikilize imla inayojumuisha maneno yaliyo na herufi za sauti lengwa na kuyaandika. | |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Maamkuzi ya nyakati za siku. (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yatumiwayo katika maamkuzi ya nyakati za siku shuleni kwa mawasiliano mwafaka<br>b) kuamkua na kuitikia maamkuzi ya nyakati za siku shuleni katika kuimarisha mawasiliano<br>c) kusoma maneno yanayotumiwa katika maamkuzi shuleni katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>d) kufafanua umuhimu wa salamu shuleni ili kuimarisha mawasiliano<br>e) kufurahia kuamkua wenzake, wafanyakazi na walimu shuleni katika kujenga mshikamano wa jamii. | • Mwanafunzi aigize maamkuzi mbalimbali ya nyakati za siku k.m habari ya asubuhi, jioni, mchana, umeamkaje na umeshindaje.<br>• Mwanafunzi aweza kuonyeshwa mchoro wa watu wawili wakisalimiana halafu aongozwe katika kujadili picha.<br>• Wanafunzi wasalimiane na kisha washirikishwe katika mjadala kuhusu maamkuzi.<br>• Wanafunzi waweza kuwekwa katika vikundi ili wajadili umuhimu wa maamkuzi.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video inayoonyesha watu wakitumia maamkuzi ya nyakati za siku.<br>• Mwanafunzi asome maamkuzi ya nyakati za siku katika kadi na chati. | 1) Tunaamkuana vipi wakati wa asubuhi, mchana na jioni?<br>2) Kwa nini tunasalimiana shuleni? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Msamiati<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua kwa kutaja msamiati wa shuleni katika kuimarisha umilisi wa lugha<br>b) kutumia msamiati wa shuleni katika mawasiliano ya kila siku<br>c) kusoma maneno na sentensi zinazojumuisha msamiati wa shuleni katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>d) kuandika maneno na sentensi fupi kuhusu shule ili kuimarisha stadi ya kuandika<br>e) kufurahia kutumia msamiati wa shule katika mawasiliano ya kila siku. | • Mwanafunzi aonyeshwe vifaa halisi, picha au michoro ya vitu vinavyopatikana shuleni kama vile ofisi, maktaba, vyoo, darasa, bendera na gwaride.<br>• Mwanafunzi achore maumbo ya vifaa vinavyopatikana shuleni.<br>• Wanafunzi waambatanishe kadi za maneno na vifaa halisi wakiwa katika vikundi.<br>• Wanafunzi waweza kushiriki katika nyimbo na mashairi kuhusu shule.<br>• Mwanafunzi aandike majina ya vitu vinavyopatikana shuleni.<br>• Mwanafunzi asome msamiati wa shuleni katika kadi au chati.<br>• Mwanafunzi atunge na asoma sentensi akitumia msamiati wa shuleni. | 1) Je, unajua vifaa gani vinavyopatikana shuleni?<br>2) Taja vifaa mbalimbali vinavyopatikana shuleni na umuhimu wake. |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutaja majina ya vitu vinavyopatikana shuleni ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>b) kuelezea vitu vinavyopatikana shuleni ili kuimarisha stadi ya kusikiliza<br>c) kusikiliza kwa makini masimulizi ili kuimarisha stadi ya kusikiliza<br>d) kusimulia kuhusu vitu mbalimbali vinavyopatikana shuleni ili kuimarisha stadi ya kusikiliza | • Mwanafunzi asimulie kisa kuhusu shule.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika mjadala kuhusu vifaa vinavyopatika shuleni.<br>• Mwanafunzi afafanue umuhimu wa vitu vinavyopatika shuleni.<br>• Mwanafunzi aweza kushiriki katika nyimbo au mashairi kuhusu vifaa vinavyopatika shuleni.<br>• Mwanafunzi atazame picha na michoro inayoonyesha vifaa vinavyopatika shuleni wajadiliane katika vikundi. | 1) Ni vifaa vipi vinavyopatikana shuleni?<br>2) Ni nani anayetumia vifaa hivyo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | e) kuthamini umuhimu wa vitu vinavyopatikana shuleni. | | |
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua picha za vitu vinavyopatikana shuleni katika kujenga stadi ya kusoma<br>b) kuelezea picha katika hadithi ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>c) kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu kuhusu vitu vinavyopatikana shuleni ili kuimarisha umakinifu<br>d) kusoma hadithi kuhusu shule ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>e) kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa katika kupata mafunzo ya hadithi<br>f) kuchangamkia kusoma hadithi kuhusu shule. | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi asikize mwalimu anaposoma hadithi kisha asome pamoja na mwalimu na baadaye asome peke yake kwa sauti.<br>• Wanafunzi wasomeane hadithi wakiwa wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kwenye vifaa vya teknolojia k.v. tarakilishi na kinasasauti na kufuatilia yanayosomwa kwenye projekta.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kutoka kwa jitabu mbele ya darasa.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma hadithi.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali yanayotokana na hadithi aliyosoma na kusomewa.<br>• Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa. | 1) Unaona nini katika picha?<br>2) Ni nini kitatendeka katika hadithi?<br>3) Ni nani wahusika katika hadithi? |
| | Msamiati: Nambari 11-50 (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nambari 11-50 kwa maneno ili kuimarisha mawasiliano | • Mwanafunzi asome majina ya nambari 11-50.<br>• Wanafunzi wasome kadi za nambari 11-50 na majina yake ili kuziambatanisha katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aandike nambari 11-50. | 1) Andika nambari gani kati ya 11 hadi 50?<br>2) Taja 11-50 kwa Kiswahili. |

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko na maadili:**<br>uraia – utangamano wa kijamii<br>wanafunzi watangamane na kufanya kazi pamoja. | **Uhusiano na Maadili:**<br>Uwajibikaji. |
| **Uhusiano na masomo mengine:** English Activities, Literacy and Indigenous Languages, Environmental activities. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>kuwahamasisha wengine katika jamii kuhusu umuhimu wa shule. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>• kazi ya vikundi<br>• michezo<br>• nyimbo na mashairi kuhusu usafi wa mwili. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kuuliza maswali kuhusu shuleni<br>• kuchunguza anavyotamka sauti zilizofunzwa<br>• kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa<br>• kuchunguza jinsi anavyotumia **–ako** na **-enu** katika sentensi. |

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti lengwa kwa ukakamavu na ufasaha<br>• anatumia msamiati wa shuleni katika sentensi ifaavyo na kwa ubunifu<br>• anasoma kwa ufasaha<br>• anatumia nambari kumi na moja hadi hamsini kwa ubunifu katika sentensi<br>• anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi | Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti lengwa vyema<br>• anatumia msamiati wa shuleni ifaavyo katika sentensi<br>• anasoma ifaavyo.<br>• anatumia nambari kumi na moja hadi hamsini ifaavyo katika sentensi<br>• anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto katika kutamka baadhi ya sauti lengwa vyema<br>• ana changamoto katika kutumia baadhi ya msamiati wa shuleni katika sentensi<br>• ana changamoto kiasi katika kusoma<br>• ana changamoto za kutumia baadhi ya nambari kutoka kumi na moja hadi hamsini katika sentensi<br>• anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto katika kutamka sauti lengwa<br>• ana changamoto katika kutumia msamiati wa shuleni katika sentensi<br>• ana changamoto nyingi katika kusoma<br>• ana changamoto za kutumia majina ya nambari kutoka kumi na moja hadi hamsini katika sentensi<br>• ana changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| • anatumia **-ako** na **-enu** kutunga sentensi ifaavyo kila wakati<br>• anaandika kwa hati nadhifu na kwa haraka. | • anatumia **-ako** na **-enu** kutunga sentensi ifaavyo<br>• anaandika kwa hati zinazosomeka. | • ana changamoto katika kutumia **-ako** na **-enu** kutunga sentensi ifaavyo<br>• anaandika kwa hati zinayosomeka. | • ana changamoto katika kutumia **-ako** na **-enu** kutunga sentensi ifaavyo<br>• ana changamoto katika kuandika. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Haki Zangu** | Sauti na majina ya herufi za Kiswahili (*Vipindi 6*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutamka sauti nne za herufi moja katika kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>b) kutambua sauti za herufi moja zilizofunzwa katika maneno ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>c) kutambua majina ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>d) kusoma herufi za sauti moja kwa ufasaha ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>e) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa kwa ufasaha ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>f) kusoma vifungu vilivyo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>g) kuandika herufi zinazowakilishwa na sauti lengwa ili kuimarisha stadi ya kuandika | • Mwanafunzi aweza kutambua sauti /p/, /f/ na /v/ katika maneno.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu akitamka sauti lengwa, kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili na kama darasa.<br>• Mwanafunzi atambue sauti alizosoma katika maneno.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia teknolojia (papaya) kusikiliza matamshi ya sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi.<br>• Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno.<br>• Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi au kwa kugawa maneno marefu katika sehemu ndogo ndogo. | 1) Ni sauti zipi unazojua kutamka?<br>2) Unajua kusoma herufi na maneno gani?<br>3) Unajua kuandika herufi na maneno gani? |

| | | | |
|---|---|---|---|
| • anatumia **-ako** na **-enu** kutunga sentensi ifaavyo kila wakati<br>• anaandika kwa hati nadhifu na kwa haraka. | • anatumia **-ako** na **-enu** kutunga sentensi ifaavyo<br>• anaandika kwa hati zinazosomeka. | • ana changamoto katika kutumia **-ako** na **-enu** kutunga sentensi ifaavyo<br>• anaandika kwa hati zinayosomeka. | • ana changamoto katika kutumia **-ako** na **-enu** kutunga sentensi ifaavyo<br>• ana changamoto katika kuandika. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Haki Zangu** | Sauti na majina ya herufi za Kiswahili<br>(*Vipindi 6*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutamka sauti nne za herufi moja katika kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>b) kutambua sauti za herufi moja zilizofunzwa katika maneno ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>c) kutambua majina ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>d) kusoma herufi za sauti moja kwa ufasaha ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>e) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa kwa ufasaha ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>f) kusoma vifungu vilivyo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>g) kuandika herufi zinazowakilishwa na sauti lengwa ili kuimarisha stadi ya kuandika | • Mwanafunzi aweza kutambua sauti /p/, /f/ na /v/ katika maneno.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu akitamka sauti lengwa, kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili na kama darasa.<br>• Mwanafunzi atambue sauti alizosoma katika maneno.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia teknolojia (papaya) kusikiliza matamshi ya sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi.<br>• Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno.<br>• Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi au kwa kugawa maneno marefu katika sehemu ndogo ndogo. | 1) Ni sauti zipi unazojua kutamka?<br>2) Unajua kusoma herufi na maneno gani?<br>3) Unajua kuandika herufi na maneno gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutaja haki zake ili kuimarisha ujuzi wa masuala yanayomwathiri<br>b) kueleza umuhimu wa haki za watoto ili kutetea haki zake zinapokiukwa<br>c) kusimulia kuhusu haki zake ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>d) kusikiliza masimulizi kuhusu haki za watoto ili kuimarisha umakinifu<br>e) kuthamini haki za watoto ili kuzitetea maishani. | • Mwanafunzi ataje haki zake k.v. kuishi, elimu, kupewa malezi bora, matibabu, kutoteswa, kupewa jina, chakula na mavazi.<br>• Wanafunzi wajadili michoro, chati au picha zinazozingatia haki za watoto.<br>• Mwanafunzi aweza kusimulia kisa kuhusu haki za watoto.<br>• Mwanafunzi aweza kuimba nyimbo na kukariri mashairi kuhusu haki za watoto.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video kuhusu haki za watoto.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza mgeni mwalikwa akizungumza kuhusu haki za watoto.<br>• Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu haki za watoto. | 1) Je, unajua haki zipi? zinazokuhusu?<br>2) Haki za watoto zinakusaidiaje? |
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua picha kuhusu haki za watoto ili kuifahamu hadithi vizuri<br>b) kusikiliza hadithi za mwalimu kuhusu haki za watoto katika kuimarisha stadi za kusikiliza na kusoma<br>c) kusoma hadithi kuhusu haki za watoto katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>d) kufahamu hadithi aliyoisoma au aliyosomewa ili kupata mafunzo yanayolengwa | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma hadithi.<br>• Mwanafunzi adhihirishe ufahamu wa matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza mwalimu anaposoma hadithi kisha asome na mwalimu na baadaye asome peke yake, wakiwa wawili wawili au katika vikundi. | 1) Ni masuala yapi uliyojifunza katika hadithi uliyosoma?<br>2) Ni haki zipi za watoto zimezingatiwa katika hadithi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | e) kuchangamkia kusoma hadithi kuhusu haki za watoto ili kuendeleza stadi ya kusoma. | • Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kwa kutumia vifaa vya kiteknolojia k.m. tarakilishi na projekta.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kutoka kwa jitabu mbele ya darasa.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali yanayotokana na hadithi aliyosoma au kusomewa.<br>• Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa. | |
| | Sarufi: Matumizi ya **vizuri** na **vibaya** (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi yafaayo ya **vizuri** na **vibaya** katika mawasiliano<br>b) kutumia **vizuri** na **vibaya** katika sentensi sahihi ili kuimarisha mawasiliano<br>c) kusoma sentensi zinazojumuisha **vizuri** na **vibaya** ili kuimarisha usomaji bora<br>d) kuandika sentensi kwa kujumuisha **vizuri** na **vibaya** ili kuimarisha uandishi mwafaka<br>e) kuchangamkia matumizi ya **vizuri** na **vibaya** katika kuimarisha mawasiliano. | • Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia **vizuri** na **vibaya.**<br>• Mwanafunzi aweza kubainisha matumizi ya vielezi lengwa kwa kutumia vifaa vya teknolojia.<br>• Mwanafunzi arejelee vitendo mbalimbali kwa kutumia **vizuri** na **vibaya** k.m Mtoto amesoma vizuri.<br>• Mwanafunzi aandike sentensi zinazojumuisha **vizuri** na **vibaya.** | 1) Unatumia maneno yapi kuelezea vile mtu alivyofanya jambo? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanashiriki katika makundi
ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko:** Uraia – haki za watoto -wanafunzi wanahamasishwa kuhusu haki zake. | **Uhusiano na Maadili:** uwajibikaji, haki za kijamii, heshima. |

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masomo mengine:** Environmental Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>kuwahamasisha wengine katika jamii kuhusu haki za watoto. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>• kazi ya vikundi<br>• michezo<br>• nyimbo na mashairi kuhusu usafi wa mwili. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kuchunguza anavyotamka sauti zilizofunzwa<br>• kuuliza maswali kuhusu haki za watoto<br>• kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa<br>• kuchunguza jinsi anavyotumia vizuri na vibaya katika sentensi. |

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti lengwa vyema na kwa ukakamavu<br>• anatambua haki za watoto na kuzitilia maanani katika mawasiliano<br>• anatumia msamiati wa haki za watoto kwa ubunifu katika sentensi<br>• anasoma kwa ufasaha<br>• anatetea haki za watoto kwa ukakamavu<br>• anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi<br>• anatumia vivumishi **vizuri** na **vibaya** kutunga sentensi ifaavyo na kwa ubunifu wa hali ya juu.<br>• anaandika kwa hati nadhifu. | Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti lengwa vyema<br>• anatambua haki za watoto<br>• anatumia msamiati wa haki za watoto ifaavyo katika sentensi<br>• anasoma ifaavyo<br>• anatetea haki za watoto<br>• anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi<br>• anatumia vivumishi **vizuri** na **vibaya** kutunga sentensi ifaavyo<br>• anaandika kwa hati bora. | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto za kutamka baadhi ya sauti lengwa vyema<br>• anatambua haki za watoto<br>• ana changamoto za kutumia baadhi ya msamiati wa haki za watoto katika sentensi<br>• anasoma baadhi ya kazi anazopewa<br>• anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi<br>• ana changamoto katika kutumia vivumishi **vizuri** na **vibaya** kutunga sentensi ifaavyo<br>• anaandika kwa hati zinazosomeka. | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto za kutamka sauti lengwa<br>• ana changamoto katika kutambua haki za watoto<br>• ana changamoto za kutumia msamiati wa haki za watoto katika sentensi<br>• ana changamoto katika kusoma kazi anazopewa<br>• ana changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi<br>• ana changamoto za kutumia vivumishi **vizuri** na **vibaya** kutunga sentensi ifaavyo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | • ana changamoto katika kusoma. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Usafiri** | Sauti za herufi mbili za Kiswahili<br>(*Vipindi 4*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti za herufi mbili zilizofunzwa ili kuimarisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza<br>b) kutamka sauti lengwa za herufi mbili katika kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>c) kusoma herufi za sauti mbili ili kuimarisha usomaji bora<br>d) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha usomaji bora<br>e) kusoma hadithi fupi zilizo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kuimarisha usomaji bora<br>f) kuandika maneno kutokana na herufi alizofunzwa ili kuimarisha stadi ya kuandika<br>g) kufurahia kutumia sauti zilizofunzwa katika mawasiliano. | • Mwanafunzi atambue sauti /ch/ na /dh/ katika maneno.<br>• Mwanafunzi asikilize sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili na kama darasa.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia vifaa vya kiteknolojia kama vile papaya na DVD kusikiliza sauti zikitamkwa.<br>• Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi.<br>• Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno.<br>• Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi aandike herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni.<br>• Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi na kuchanganua yaliyo marefu zaidi.<br>• Wanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta na kipasasauti na rununu kusikiliza na kusoma hadithi. | 1) Ni sauti zipi unazojua kutamka?<br>2) Unajua kusoma silabi na maneno yapi?<br>3) Unajua kuandika silabi na maneno yapi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aweza kufinyanga maumbo ya herufi inayowakilisha sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi anakili herufi na maneno yanayotokana na sauti alizofunzwa. | |
| | Msamiati<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua baadhi ya majina ya vyombo vya usafiri katika kuimarisha mawasiliano<br>b) kusoma majina ya vyombo vya usafiri na msamiati mwingine wa usafiri katika sentensi ili kuimarisha usomaji bora<br>c) kutumia msamiati wa usafiri kutungia sentensi katika kuimarisha stadi ya kuzungumza na kuandika<br>d) kuandika majina ya vyombo vya usafiri na msamiati mwingine wa usafiri ili kuimarisha stadi ya kuandika<br>e) kuthamini vyombo vya usafiri katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia msamiati wa vyombo vya usafiri k.v matatu, basi, lori, pikipiki, garimoshi, gari dogo, ndege na meli.<br>• Mwanafunzi atoe maana ya msamiati unaohusu usafiri.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama michoro na picha zinazolenga usafiri.<br>• Mwanafunzi achore baadhi ya vyombo vya usafiri na kuvitambua kwa majina<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video kuhusu shughuli za usafiri.<br>• Wanafunzi wajadiliane kuhusu umuhimu wa vyombo vya usafiri. | 1) Umewahi kutumia chombo kipi cha kusafiria?<br>2) Unajua vyombo gani vingine vya usafiri?<br>3) Je, ni maneno gani yanayotumiwa usafiri? |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua kwa kutaja vyombo mbalimbali vya usafiri ili kuimarisha mawasiliano | • Mwanafunzi atambue aina mbalimbali za vyombo vya usafiri k.v. matatu, basi, lori, pikipiki, garimoshi, gari dogo, ndege na meli kwa kutumia picha au vyombo vya kiteknolojia.<br>• Mwanafunzi asimulie kuhusu vyombo vya usafiri, kwa mfano; Mimi nilisafiri kwa matatu. | 1) Je, ni safari gani umewahi kufanya?<br>2) Je, unasafiria chombo gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | b) kuzungumza kuhusu vyombo vya usafiri ili kuimarisha uwezo wa kujieleza<br>c) kusikiliza visa kuhusu usafiri ili kuimarisha umakinifu<br>d) kusikiliza kisa kuhusu usafiri ili kuimarisha ukakamavu katika kujieleza<br>**e)** kufurahia masimulizi kuhusu vyombo vya usafiri ili kuimarisha mawasiliano. | • Mwanafunzi ashiriki katika mjadala darasani au katika vikundi kuhusu vyombo mbalimbali vya usafiri.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza masimulizi kuhusu vyombo vya usafiri kwa kutumia video au kinasa sauti. | |
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua picha za vyombo mbalimbali vya usafiri ili kuimarisha ufahamu wa hadithi<br>b) kuelezea maana ya maneno yaliyotumiwa katika hadithi ili kuimarisha ufahamu wa hadithi<br>c) kusikiliza hadithi inaposomwa na mwalimu ili kuimarisha umakinifu<br>d) kusoma hadithi zinazohusu usafiri kujenga stadi ya kusoma<br>e) kufahamu hadithi aliyoisoma kuhusu usafiri ili kupata ujumbe katika hadithi<br>f) kuchangamkia kusoma hadithi katika maisha ya kila siku ili | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi<br>• Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza mwalimu anaposoma hadithi kisha asome na mwalimu na baadaye asome peke yake, wakiwa wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi asimulie hadithi aliyoisoma au kusomewa kwa kutumia maneno yake mwenyewe.<br>• Mwanafunzi aweza kurekodiwa akisoma vizuri kwa video au kinasa sauti ili wanafunzi waweze kutazama na kusikiliza jinsi ya kusoma hadithi kwa ufasaha.<br>• Mwanafunzi aweza kufanya ziara ya kwenda kuona vyombo vya usafiri kwenye vituo vya usafiri.<br>• Mwanafunzi ajibu maswali ya ufahamu akiwa peke yake, wawili wawili au katika vikundi. | 1) Umewahi kusoma hadithi ipi?<br>2) Ni hadithi ipi iliyokufurahisha zaidi?<br>3) Unamkumbuka mhusika gani katika hadithi uliyosoma? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kujenga ari ya usomaji huru. | | |
| | Sarufi:<br>Matumizi ya herufi kubwa<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kubainisha matumizi ya herufi kubwa ili kuimarisha mawasiliano andishi<br>b) kusoma sentensi zilizo na matumizi ya herufi kubwa katika kuimarisha stadi za kusoma na kuandika<br>c) kuandika sentensi akitumia herufi kubwa katika kuimarisha uandishi bora<br>d) kuthamini matumizi ya herufi kubwa katika kufanikisha mawasiliano. | • Mwanafunzi aelezee matumizi ya herufi kubwa.<br>• Wanafunzi waweza kushirikishwa kusoma sentensi zinazotumia herufi kubwa wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aweza kutofautisha kati ya herufi ndogo na herufi kubwa.<br>• Mwanafunzi aakifishe sentensi kwa kutumia herufi kubwa.<br>• Wanafunzi waweza kuakifisha sentensi mbali mbali wakitumia herufi kubwa wakiwa wawili wawili au katika vikundi. | 1) Je, herufi kubwa hutumiwa wapi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanashiriki katika vikundi
ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza
hamu ya kujifunza: mwanafunzi atapata hamu ya kutaka kutumia vipengee vilivyofunzwa vya sarufi kwenye mawasiliano
ubunifu – mwanafunzi anatumia ubunifu katika kutunga sentensi na masimulizi.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala Mtambuko:**<br>elimu ya maendeleo endelevu- usalama katika usafiri –wanashughulikia vyombo vya usafiri. | **Uhusiano na Maadili:**<br>uwajibikaji<br>heshima. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>Environmental Activities; English Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>kuwahamasisha wengine kuhusu usalama barabarani. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>• kazi ya vikundi<br>• michezo | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kuchunguza anavyotamka sauti zilizofunzwa<br>• kuuliza maswali kuhusu vyombo vya usafiri<br>• kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa<br>• kuchunguza jinsi anavyotumia herufi kubwa kuakifisha maneno na sentensi. |

Compiled and Distributed by Schools Net Kenya | P.O.BOX 85726 – 00200, NAIROBI |
Mob: 0725788400 | Email:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti lengwa kwa ufasaha<br>• anataja majina ya vyombo vya usafiri kwa wepesi<br>• anatumia msamiati wa usafiri kwa ubunifu katika sentensi<br>• anasoma kwa ufasaha.<br>• anafahamu kwa urahisi hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa<br>• anatumia herufi kubwa ipasavyo katika kuakifisha maneno na sentensi kwa wakati<br>• anaandika kwa hati nadhifu na kwa haraka. | Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti lengwa vyema<br>• anataja majina ya vyombo vya usafiri<br>• anatumia msamiati wa usafiri ifaavyo katika sentensi<br>• anasoma ifaavyo<br>• anafahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa<br>• anatumia herufi kubwa ipasavyo katika kuakifisha maneno na sentensi<br>• anaandika kwa hati bora. | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto za kutamka baadhi ya sauti lengwa vyema<br>• anataja baadhi ya majina ya vyombo vya usafiri<br>• ana changamoto za kutumia baadhi ya msamiati wa usafiri katika sentensi<br>• anasoma baadhi ya kazi anazopewa<br>• anafahamu baadhi ya hadithi alizosimuliwa, aliyosoma au kusomewa<br>• ana changamoto za kutumia herufi kubwa katika kuakifisha maneno na sentensi<br>• anaandika kwa hati zinazosomeka. | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto za kutamka sauti lengwa<br>• ana changamoto ya kutaja baadhi ya majina ya vyombo vya usafiri<br>• ana changamoto za kutumia msamiati wa usafiri katika sentensi<br>• ana changamoto katika kusoma<br>• ana changamoto katika kufahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma au kusomewa<br>• ana changamoto za kutumia herufi kubwa katika kuakifisha maneno na sentensi<br>• ana changamoto katika kuandika. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Familia** | Sauti za herufi mbili za Kiswahili (*Vipindi 6*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti za herufi mbili zilizofunzwa ili kuimarisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza<br>b) kutamka sauti lengwa za herufi mbili katika kuimarisha stadi ya | • Mwanafunzi atambue sauti /gh/, /ny/ na /ng'/ katika maneno.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu akitamka sauti lengwa /gh/, /ny/ na /ng'/ kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili na kama darasa.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia teknolojia kama vile | 1) Unaweza kutamka sauti zipi ulizofunzwa awali?<br>2) Unaweza kutambua sauti gani za herufi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kuzungumza<br>c) kusoma herufi za sauti mbili ili kuimarisha usomaji bora<br>d) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha usomaji bora<br>e) kusoma hadithi fupi zilizo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kuimarisha usomaji bora<br>f) kuandika maneno kutokana na herufi alizofunzwa ili kuimarisha stadi ya kuandika<br>g) kufurahia kutumia sauti zilizofunzwa katika mawasiliano. | papaya kusikiliza sauti lengwa ikitamkwa.<br>• Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi.<br>• Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno.<br>• Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi aandike herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni.<br>• Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi na kuchanganua yaliyo marefu zaidi.<br>• Wanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta na kipasa sauti kusikiliza na kusoma hadithi.<br>• Mwanafunzi aweza kufinyanga maumbo ya herufi inayowakilisha sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi anakili herufi na maneno yanayotokana na sauti alizofunzwa. | mbili katika maneno?<br>3) Unaweza kuunda maneno yapi kwa kutumia sauti za herufi mbili? |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Maneno ya heshima na adabu. (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno ya heshima na adabu ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>b) kutumia maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano | • Mwanafunzi aelezee matumizi ya maneno ya heshima na adabu k.v. hodi, karibu, naomba, nisamehe na nashukuru.<br>• Wanafunzi waigize vitendo vya heshima na adabu wakiwa wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi atazame michoro na picha ya watu wakidhihirisha vitendo vya heshima na adabu. | 1) Unapotaka kuingia ndani ya nyumba ya jirani unafanyaje?<br>2) Mgeni anapobisha mlango unaitikia vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | c) kuonyesha vitendo vya heshima na adabu anapowasiliana katika mazingira yake<br>d) kuthamini matumizi ya maneno ya heshima na adabu katika mazingira yake. | • Wanafunzi wajadili maneno ya heshima na adabu katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video inayowasilisha vitendo vya heshima na adabu.<br>• Mwanafunzi asome maneno ya heshima na adabu.<br>• Mwanafunzi aelezee maneno ya heshima na adabu. | 3) Mtu akikutendea wema unamwambiaje?<br>4) Ukifanya kosa utasemaje? |
| | Msamiati (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutumia msamiati wa familia katika mawasiliano ya kila siku<br>b) kutunga sentensi akitumia msamiati wa familia uliofunzwa ili kuimarisha stadi ya mazungumzo na uandishi<br>c) kusoma maneno na sentensi kuhusu familia ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>d) kuandika maneno na sentensi kuhusu familia ili kuimarisha stadi ya kuandika<br>e) kufurahia kuwarejelea watu wa familia kwa majina yao mwafaka ili kuimarisha mawasiliano. | • Mwanafunzi ataje majina ya watu wa familia k.v babu, nyanya, mjomba, ami/amu, shangazi, binamu na halati.<br>• Mwanafunzi atazame picha au michoro ya watu wa familia.<br>• Wanafunzi wasome majina ya watu wa familia kwenye kadi au chati.<br>• Wanafunzi waweza kushiriki katika nyimbo na mashairi kuhusu watu wa familia.<br>• Mwanafunzi aandike majina ya familia.<br>• Mwanafunzi asome msamiati wa watu wa familia katika kadi au chati.<br>• Mwanafunzi atunge na kusoma sentensi akitumia msamiati wa familia. | 1) Wazazi wa baba/mama wanaitwaje?<br>2) Dada yake mama anaitwaje?<br>3) Dada yake baba anaitwaje?<br>4) Kaka yake baba anaitwaje?<br>5) Wtoto wa amu/ami na shangazi anaitwaje? |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutaja majina ya watu wa familia katika kujenga umilisi wa kuzungumza | • Mwanafunzi arejelee watu wa karibu katika familia aliofunzwa awali.<br>• Mwanafunzi asimulie kuhusu familia.<br>• Mwanafunzi azungumzie kuhusu familia.<br>• Mwanafunzi aelezee maana ya majina ya watu wa familia. | 1) Je, familia yenu ina watu wangapi?<br>2) Je, unajua majina gani ya watu wa familia yako? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | b) kusikiliza kwa makini masimulizi kuhusu watu wa familia ili kujenga umakinifu<br>c) kuelezea kuhusu watu wa familia katika kuimarisha uwezo wa kuwaelezea watu katika mazingira yake<br>d) kuthamini umuhimu wa familia katika kuendeleza mshikamano wa kijamii. | • Mwanafunzi aweza kushirikishwa katika nyimbo au mashairi kuhusu watu wa familia.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video picha au michoro inayoonyesha watu wa familia ili wajadiliane katika vikundi. | |
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua picha za watu wa familia ili kuimarisha ufahamu wa hadithi<br>b) kusikiliza hadithi za mwalimu kuhusu watu wa familia ili kuimarisha umakinifu<br>c) kusoma hadithi kuhusu watu wa familia ili kuimarisha usomaji bora<br>d) kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa ili kupata ujumbe<br>e) kuchangamkia kusoma hadithi kuhusu watu wa familia katika kujenga ari ya usomaji bora. | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu anaposoma hadithi kisha asome na mwalimu na baadaye asome peke yake, wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kwa kutumia tarakilishi na projekta.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kutoka kwa jitabu mbele ya darasa.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma hadithi.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kutokana na hadithi.<br>• Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa. | 1) Unaweza kutambua watu gani katika picha?<br>2) Hadithi inahusu watu gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | Sarufi: Matumizi ya maneno yanayoashiria vitendo (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua maneno yanayoashiria vitendo ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kusoma maneno yanayoashiria vitendo ili kujenga usomaji bora<br>c) kutumia maneno yanayoashiria vitendo katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano<br>d) kuandika sentensi sahihi akitumia maneno yanayoashiria vitendo katika kuimarisha uandishi bora<br>e) kufurahia kutumia maneno yanayoashiria vitendo katika mawasiliano. | • Mwanafunzi aweza kuigiza vitendo k.m. simama, tembea, andika, cheka n.k.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi zenye matumizi ya maneno yanayoashiria vitendo kwa mfano simama, oga, chana n.k.<br>• Mwanafunzi asome sentensi zinazohusisha vitendo.<br>• Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa maneno yanayoashiria vitendo.<br>• Mwanafunzi anakili sentensi kwa kutumia maneno yanayoashiria vitendo.<br>• Wanafunzi watunge sentensi katika makundi.<br>• Mwanafunzi aandike sentensi zinazohusisha vitendo.<br>• Mwanafunzi aweza kupewa zoezi la kujaza mapengo kwa tarakilishi (mchezo wa kuburura na kutia kapuni). | 1) Je, unajua kutumia maneno yapi yanayowakilisha vitendo?<br>2) Je, unajua kutumia maneno yapi yanayowakilisha vitendo katika sentensi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
mawasiliano na ushirikiano – kujadiliana kuhusu majukumu ya watu wa familia; kufanya kazi kwa makundi
ujuzi wa kidijitali : kuna mapendekezo ya kutumia vifaa vya teknolojia kufunzia
ubunifu: utunzi wa sentensi kwa kutumia **huyu** na **nani**.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>Uraia: uzalendo: kushirikiana katika vikundi; utangamano wa kijamii - mahusiano katika familia. | **Mahusiano na Maadili:**<br>mapenzi katika familia<br>heshima. |
| **Uhusiano na masomo mengine:** Religious Studies, English Activities na Environmental Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>kuwarejelea watu wa familia kwa majina yao mwafaka nyumbani<br>kuwahamasisha wengine kuhusu umuhimu wa familia<br>kuwatembelea mayatima. |

| | |
|---|---|
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>kazi ya vikundi<br>shughuli za vikundi vya ushirika shuleni<br>michezo. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kusikiliza jinsi anavyotamka sauti lengwa<br>• kuchunguza jinsi anavyowatambua watu katika familia yake.<br>• kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa<br>• kumpa zoezi ili mwanafunzi atambue vitenndo katika sentensi. |

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anawaelezea watu wa familia.<br>• anatumia majina ya watu wa familia kwa ubunifu katika sentensi<br>• anatumia maneno ya heshima kwa ubunifu katika mazungumzo<br>• anasoma kwa ufasaha<br>• anafahamu kwa urahisi hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa<br>• anatambua vitendo katika sentensi<br>• anaandika kwa hati nadhifu na kwa haraka. | Mwanafunzi,<br>• anawataja watu wa familia<br>• anatumia majina ya watu wa familia katika sentensi ifaavyo<br>• anatumia maneno ya heshima ifaavyo katika mazungumzo.<br>• anasoma ifaavyo<br>• anafahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa<br>• anatambua vitendo katika sentensi<br>• anaandika kwa hati bora. | Mwanafunzi,<br>• anawataja watu wa familia<br>• ana changamoto katika kutumia baadhi ya majina ya watu wa familia katika sentensi<br>• anasoma baadhi ya kazi anazopewa<br>• anafahamu baadhi ya hadithi alizosimuliwa, aliyosoma au kusomewa<br>• anatambua vitendo katika sentensi<br>• anaandika kwa hati zinazosomeka. | Mwanafunzi,<br>• anawataja watu wa familia<br>• ana changamoto katika kutumia majina ya watu wa familia katika sentensi<br>• ana changamoto ya kusoma.<br>• ana changamoto katika kufahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa<br>• ana changamoto nyingi katika kutambua vitendo katika sentensi<br>• ana changamoto katika kuandika. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **Usalama Wangu** | Sauti na herufi mbili za Kiswahili (*Vipindi 4*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti za herufi mbili katika kuimarisha matamshi bora<br>b) kutamka sauti za Kiswahili za herufi mbili katika kuimarisha matamshi bora<br>c) kusoma silabi za sauti zinazoundwa kutokana na sauti mbili ili kuimarisha usomaji<br>d) kuunda silabi na maneno kwa kutumia sauti lengwa katika kuimarisha umilisi wa kusoma maneno<br>e) kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>f) kusoma hadithi fupi zilizo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>g) kuandika maneno kutokana na herufi za sauti lengwa katika kuimarisha uandishi<br>h) kufurahia kutumia sauti zilizofunzwa katika mawasiliano. | • Mwanafunzi atambue sauti /sh/na /th/ katika maneno<br>• Mwanafunzi asikilize sauti lengwa ikitamkwa na mwalimu kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili na kama darasa nzima.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia vifaa vya kiteknolojia kama vile papaya, tarakilishi na projekta kusikiliza sauti lengwa ikitamkwa.<br>• Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi.<br>• Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno.<br>• Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa mwenye umahiri katika kutamka sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi asome maneno kwa kuyagawa maneno marefu katika sehemu ndogo ndogo.<br>• Wanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aweza kufinyanga maumbo ya herufi inayowakilisha sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi anakili herufi na maneno yanayotokana na sauti alizofunzwa.<br>• Mwanafunzi aandike herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni. | 1) Je, sauti /sh/ na /th/ hutamkwa vipi?<br>2) Je, ni maneno kama gani ambayo yana sauti /sh /na /th /? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Msamiati (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua msamiati ambao hutumiwa katika usalama ili kuwasiliana kuhusu masuala yanayohusu usalama wake<br>b) kueleza maana ya msamiati wa usalama katika kuimarisha mawasiliano<br>c) kutumia msamiati wa usalama katika sentensi sahihi katika kuimarisha mawasiliano<br>d) kuthamini usalama wake katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi atoe maana ya msamiati wa usalama.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati wa usalama kama vile, kivukio cha barabara, moto, vidaraja, ajali michezoni, kuzama majini na vita.<br>• Wanafunzi waweza kuchora baadhi ya vifaa vinavyohusiana na usalama wao kama vile kivukio cha barabarani vidaraja.<br>• Wanafunzi waweza kutazama video, michoro au picha zinazolenga usalama wao.<br>• Wanafunzi wajadiliane kuhusu umuhimu wa usalama wao kwenye makundi. | 1) Unaweza kutaja mambo gani yanayohusu usalama?<br>2) Ni ajali gani ambayo umewahi kushuhudia au kuelezewa?<br>3) Unawezaje kuepuka ajali? |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua jinsi ya kuepukana na baadhi za ajali katika mazingira yao<br>b) kujiepusha na vitendo vinavyoweza kumdhuru maishani<br>c) kusimulia kuhusu mambo yanayoweza kuhatarisha usalama wake ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>d) kusikiliza masimulizi kuhusu usalama wa watoto katika kujenga umakinifu<br>e) kuthamini umuhimu wa usalama wake katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi asimulie baadhi ya mambo yanayoweza kuhatarisha usalama wake kupitia kwa mgeni mwalikwa.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video, picha au michoro inayoashiria usalama wa watoto.<br>• Wanafunzi wajadiliane kuhusu usalama wao katika vikundi.<br>• Wanafunzi waigize namna ya kuepuka ajali mbalimbali kama vile moto, kuvunjika viungo, kugongwa barabarani na kupigana.<br>• Mwanafunzi aandike baadhi ya mambo muhimu kuhusu usalama wake. | 1) Ni nini maana ya ajali?<br>2) Je, ajali mbalimbali husababishwa na nini?<br>3) Ni ajali gani umewahi kushuhudia katika shughuli za kila siku?<br>4) Unawezaje kuepuka ajali? |
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua picha zinazohusu usalama ili | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi | 1) Je, umesoma hadithi ngapi?<br>2) Ni hadithi ipi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kuimarisha ufahamu wa hadithi<br>b) kusoma hadithi kuhusu usalama ili kujenga stadi ya kusoma<br>c) kusikiliza hadithi inayosomwa na mwalimu kuhusu usalama ili kujenga usikivu wake<br>d) kufahamu hadithi aliyoisoma au kusomewa kuhusu usalama wake ili kupata ujumbe wa hadithi<br>e) kuchangamkia kusoma hadithi kila siku. | • Mwanafunzi adhihirishe ufahamu wa matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu anaposoma hadithi kisha asome na mwalimu na baadaye asome peke yake, wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kwa kutumia tarakilishi na projekta.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kutoka kwa jitabu mbele ya darasa.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma hadithi.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kutokana na hadithi.<br>• Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa. | iliyokufurahisha zaidi?<br>3) Unakumbuka nani katika hadithi iliyowahi kukufurahisha? |
| | Sarufi: Matumizi ya **Huyo** na **Hao** (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kufahamu matumizi ya **huyo** na **hao** katika mawasiliano<br>b) kutumia **huyo** na **hao** katika sentensi kwa usahihi ili kuimarisha mawasiliano<br>c) kusoma sentensi zinazojumuisha **huyo** na **hao** ili kujenga stadi ua kusoma<br>d) kuandika sentensi zinazojumuisha **huyo** na **hao** katika kuimarisha uandishi<br>e) kuchangamkia matumizi ya **huyo** na **hao** katika maawasiliano. | • Mwanafunzi asome sentensi zenye kudhihirisha matumizi ya **huyo** na **hao** kama vile: Huyo ni nani?<br>• Mwanafunzi aandike sentensi zinadhihirisha matumizi ya **huyo** na **hao** kama vile: huyo ni nani?- huyo ni kaka.<br>• Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia **huyo** na **hao.**<br>• Mwanafunzi aigize vitendo vya kuwaashiria watu mbalimbali kwa kutumia **huyo** na **hao.**<br>• Mwanafunzi aweza kukamilisha mafungu yanayohusu matumizi ya huyo na nani wakiwa wawili wawili k.m. Mtoto ____ (huyo) Watoto_____ (hao). | 1) Unatumia neno gani kuonyeshea mwenzako akiwa mbali kidogo?<br>2) Unatumia neno gani kuuliza swali kuhusu mwenzako? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

| | |
|---|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanashiriki katika vikundi.<br>ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza | |
| **Uhusiano na masuala mtambuko na maadili:**<br>elimu ya maendeleo endelevu – somo la usalama: kueleza jinsi ya kujiepusha na vitendo vinavyoweza kumdhuru maishani. | **Uhusiano na Maadili:**<br>uwajibikaji; mapenzi; uaminifu. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Environmental Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>kuwahamasisha wengine kuhusu usalama<br>kufunza wengine katika jamii kuhusu ishara za barabarani. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>Kazi ya vikundi<br>Shughuli za vikundi vya ushirika shuleni<br>Michezo | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kusikiliza jinsi anavyotamka sauti lengwa<br>• kumwuliza maswali kuhusu usalama<br>• kuchunguza anapotumia msamiati wa usalama katika sentensi<br>• kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa<br>• kumpa zoezi ili atumie **huyo** na **hao** katika sentensi. |

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti lengwa kwa ufasaha<br>• anaelezea njia mbalimbali za kudumisha usalama wake<br>• anatumia msamiati wa usalama kwa ubunifu katika sentensi ifaavyo | Mwanafunzi,<br>• anatamka sauti lengwa ipasavyo<br>• anataja njia mbalimbali za kudumisha usalama wake<br>• anatumia msamiati wa usalama katika sentensi ifaavyo | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto katika kutamka baadhi ya sauti lengwa<br>• anataja njia kadhaa za kudumisha usalama wake<br>• ana changamoto za kutumia baadhi ya msamiati wa usalama katika sentensi<br>• anasoma baadhi ya herufi, silabi na | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto katika kutamka sauti lengwa<br>• ana changamoto katika kutaja njia za kudumisha usalama wake<br>• ana changamoto za kutumia msamiati wa usalama katika sentensi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| • anasoma kwa ufasaha<br>• anafahamu kwa urahisi hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa<br>• anatumia **huyo** na **hao** katika sentensi kwa usahihi kila wakati<br>• anaandika kwa hati nadhifu na kwa haraka. | • anasoma ifaavyo<br>• anafahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa<br>• anatumia **huyo** na **hao** katika sentensi kwa usahihi<br>• anaandika kwa hati bora. | maneno<br>• anafahamu baadhi ya hadithi alizosimuliwa, aliyosoma au kusomewa<br>• ana changamoto katika kutumia **huyo** na **hao** katika sentensi kwa usahihi<br>• anaandika kwa hati zinazosomeka. | • ana changamoto katika kusoma<br>• ana changamoto katika kufahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosomoma na kusomewa<br>• ana changamoto katika kutumia **huyo** na **hao** katika sentensi kwa usahihi<br>• ana changamoto katika kuandika. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Hali ya Anga** | Alfabeti ya Kiswahili<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua alfabeti ya Kiswahili ili kuimarisha usomaji<br>b) kusoma alfabeti ya Kiswahili kwa mfuatano ufaao katika kuimarisha matumizi ya kamusi baadaye<br>c) kubainisha irabu za Kiswahili ili kuelewa jinsi silabi huundwa<br>d) kubainisha konsonanti za Kiswahili ili kuelewa jinsi silabi huundwa<br>e) kuandika alfabeti ya Kiswahili katika kuimarisha uandishi bora<br>f) kuthamini alfabeti katika | • Mwanafunzi asome alfabeti ya Kiswahili kwa mfuatano: a, b, ch, d, dh, e, f, g, gh, h, i, j, k, l, m, n, ng', ny, o, p, r, s, sh, t, th, u, v, w, y, z.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma alfabeti kwenye chati.<br>• Mwanafunzi aweza kuimba wimbo wa alfabeti.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza alfabeti ya Kiswahili ikikaririwa kwenye vifaa vya kiteknolojia kama vile kinasasauti.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika kikundi ili kutenganisha konsonanti na irabu akitumia kadi za herufi.<br>• Mwanafunzi aandike alfabeti ya Kiswahili.<br>• Wanafunzi washiriki katika mjadala kuhusu umuhimu wa alfabeti katika lugha. | 1) Je, lugha ya Kiswahili ina herufi ngapi?<br>2) Je, ni herufi gani unazoweza kusoma?<br>3) Alfabeti ni nini?<br>4) Lugha ya Kiswahili ina konsonanti ngapi?<br>5) Lugha ya Kiswahili ina irabu ngapi?<br>6) Je, irabu na konsonanti hutofautianaje katika alfabeti?<br>7) Alfabeti ina umuhimu upi katika lugha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | lugha. | | |
| | Msamiati (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati ambao hutumiwa katika hali ya anga ili kuelezea hali ya anga ifaavyo<br>b) kutambua hali ya anga ya siku husika ili kuimarisha mawasiliano<br>c) kueleza maana ya msamiati unaohusu hali ya anga katika kuimarisha stadi ya kuzungumza na kuandika<br>d) kutumia msamiati unaohusu hali ya anga katika sentensi sahihi ili kuimarisha stadi ya kuzungumza na kuandika<br>e) kuthamini hali mbalimbali za anga ili kuielewa misimu. | • Mwanafunzi atoe maana ya msamiati unaohusu hali ya anga.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia msamiati unaohusu hali ya anga kama vile upepo, jua, mvua na mawingu.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video inayoonyesha hali mbalimbali za anga.<br>• Mwanafunzi atazame michoro na picha zinazolenga hali mbambali za anga.<br>• Mwanafunzi achore baadhi ya michoro inayoashiria hali mbalimbali za hali ya anga kama vile mvua, mawingu na jua.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika mjadala kuhusu umuhimu wa hali mbalimbali za anga. | 1) Je, ni vipi unavyoweza kuelezea upepo?<br>2) Ni hali ya anga ipi inayokufurahisha zaidi?<br>3) Mvua hutusaidia vipi? |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati unaotumika kuonyesha hali ya anga ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kubainisha hali mbalimbali za anga ili kuimarisha | • Mwanafunzi asimulie visa kuhusu hali mbalimbali za anga.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video inayohusu hali ya anga.<br>• Wanafunzi waweza kupewa nafasi kwenda nje ya darasa na kujadiliana kuhusu hali ya anga wakati huo.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika majadiliano kuhusu hali | 1) Anga ni nini?<br>2) Je, ni vitu vipi hupatikana angani?<br>3) Dalili ya mvua ni nini?<br>4) Mvua hutusaidiaje?<br>5) Unaona nini katika chati ya hali ya anga? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | mawasiliano<br>c) kusimulia kuhusu hali mbalimbali za anga ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>d) kusikiliza masimulizi kuhusu hali ya anga ili kujenga umakinifu<br>e) kuthamini umuhimu wa hali ya anga katika maisha ya kila siku. | za anga tofauti kama vile upepo, jua, mvua na mawingu katika makundi.<br>• Mwanafunzi aelezee hali mbalimbali za anga kwa kutumia michoro au picha . | |
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua picha za kuonyesha hali ya anga ili kuimarisha ufahamu<br>b) kutambua maneno yanayohusiana na hali ya anga ili kuimarisha usomaji<br>c) kusoma hadithi zinazohusu hali ya anga ili kuimarisha usomaji<br>d) kusikiliza hadithi za mwalimu kuhusu hali ya anga ili kujenga stadi ya kusoma na kusikiliza<br>e) kufahamu hadithi aliyoisoma kuhusu hali ya anga ili kupata ujumbe<br>f) kuchangamkia kusoma hadithi katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu anaposoma hadithi kisha asome na mwalimu na baadaye asome peke yake, wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kwa kutumia tarakilishi na projekta.<br>• Mwanafunzi asome hadithi kutoka kwa jitabu mbele ya darasa.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kutoka kwa kitabu cha hadithi.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma hadithi.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kutokana na | 1) Je, ni hadithi zipi ambazo umewahi kusoma?<br>2) Kati ya hadithi hizo, ni ipi iliyokufurahisha zaidi?<br>3) Unakumbuka nani katika hadithi hiyo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | hadithi.<br>• Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa. | |
| | Sarufi: Nafsi ya pili wakati uliopita (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno na viambishi vinavyowakilisha nafsi ya pili wakati uliopita ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kusoma vifungu vya maneno yanayoashiria nafsi ya pili wakati uliopita ili kuimarisha usomaji<br>c) kutumia nafsi ya pili wakati uliopita hali ya umoja na wingi katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano<br>d) kuandika vifungu vya maneno vinavyoashiria nafsi ya pili wakati uliopita katika hali ya umoja na wingi ili kuimarisha uandishi bora<br>e) kufurahia kutumia nafsi ya pili wakati uliopita hali ya umoja na wingi katika mawasiliano. | • Mwanafunzi atumie nafsi ya pili wakati uliopita hali ya umoja na wingi katika mazungumzo.<br>• Mwanafunzi atumie nafsi ya pili wakati uliopita hali ya umoja na wingi katika sentensi.<br>• Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia maneno na viambishi vinavyowakilisha nafsi ya pili wakati uliopita kama vile, **wewe**, **u**, **li**, **nyinyi** na **m** hali ya umoja na wingi.<br>• Mwanafunzi aigize nafsi ya pili wakati uliopita hali ya umoja na wingi katika makundi kwa kutumia mafungu kama vile wewe uliandika-nyinyi mliandika, wewe ulisoma- ninyi mlisoma.<br>• Mwanafunzi aweza kupewa zoezi katika tarakilishi ili atumie mbinu ya kuburura majibu sahihi na kutia kapuni. | 1) Je, unatumia neno gani kumzungumzia mwenzako aliye karibu?<br>2) Je, unatumia neno gani kuwarejelea wenzako wakiwa karibu?<br>3) Je, utajuaje kwamba neno lililotumiwa kurejelea kitendo limetumika katika wakati uliopita? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanashiriki katika vikundi
ujuzi wa kidijitali – matumizi ya kiteknolojia katika kujifunza.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko:** | **Uhusiano na Maadili:** uwajibikaji ; mapenzi. |

| | |
|---|---|
| elimu ya maendeleo endelevu: elimu ya mazingira – hali ya anga | |
| **Uhusiano na masomo mengine:** Environmental Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>kuwahamasisha wengine kuhusu mazingira<br>kuwahamasisha wengine jinsi ya kuvaa kutegemea hali tofauti za anga. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>kazi ya vikundi<br>shughuli za vikundi vya ushirika shuleni<br>nyimbo na Mashairi kuhusu hali tofauti za anga. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kumwuliza maswali kuhusu hali ya anga<br>• kuchunguza anapotumia msamiati wa hali ya anga katika sentensi<br>• kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa<br>• kumpa zoezi ili atumie nafsi ya pili wakati uliopita katika sentensi. |

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anatambua hali mbalimbali za anga kwa ukakamavu<br>• anatumia msamiati wa hali ya anga kwa ubunifu katika sentensi<br>• anataja alfabeti ya Kiswahili kwa ufasaha na kwa wepesi<br>• anasoma kwa ufasaha.<br>• anafahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa kila wakati<br>• anatumia nafsi ya pili wakati uliopita katika sentensi kwa usahihi kila wakati | Mwanafunzi,<br>• anatambua hali mbalimbali za anga<br>• anatumia msamiati wa hali ya anga katika sentensi ifaavyo.<br>• anataja alfabeti ya Kiswahili kwa ufasaha<br>• anasoma ifaavyo<br>• anafahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa<br>• anatumia nafsi ya pili wakati uliopita katika | Mwanafunzi,<br>• anatambua baadhi ya hali za anga<br>• ana changamoto katika kutumia baadhi ya msamiati wa hali ya anga katika sentensi<br>• anataja alfabeti ya Kiswahili<br>• anasoma baadhi ya kazi anazopewa<br>• anafahamu baadhi ya hadithi alizosimuliwa, aliyosoma au kusomewa<br>• ana changamoto katika kutumia nafsi ya pili wakati uliopita katika sentensi. | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto katika kutambua hali mbalimbali za anga<br>• ana changamoto za kutumia msamiati wa hali ya anga katika sentensi.<br>• ana changamoto katika kutaja alfabeti ya Kiswahili<br>• ana changamoto katika kusoma.<br>• ana changamoto katika kufahamu hadithi alizosimuliwa, aliyosoma au kusomewa.<br>• ana changamoto katika kutumia nafsi ya pili wakati uliopita katika sentensi.<br>• ana changamoto katika kuandika. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| • anaandika kwa hati nadhifu na kwa haraka. | sentensi kwa usahihi<br>• anaandika kwa hati bora. | • anaandika kwa hati zinazosomeka. | |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Lishe Bora** | Msamiati (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu lishe bora ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kusoma maneno yanayohusiana na lishe bora ili kuimarisha usomaji<br>c) kuandika maneno yanayohusu lishe bora katika kuimarisha uandishi bora<br>d) kutumia msamiati ulisomwa katika kutunga sentensi ili kuimarisha mawasiliano<br>e) kuthamini kula chakula kinachofaidi mwili ili kujikinga kutokana na madhara ya ukosefu wa lishe bora. | • Mwanafunzi aelezee maana ya msamiati unaohusiana na lishe bora kama vile protini, vitamini, wanga (vyakula vinavyopatia mwili nguvu) chumvi, ukosefu, upungufu na baadhi ya vyakula vinavyofaidi mwili na afya.<br>• Wanafunzi wajadiliane katika vikundi au wakiwa wawili wawili kuhusu vyakula vinavyodhuru afya.<br>• Mwanafunzi atazame kwenye vyombo vya kiteknolojia na kuvijadili picha za vyakula vinavyoashiria msamiati unaorejelewa.<br>• Mwanafunzi asome majina mbalimbali ya vyakula kwenye kadi za maneno.<br>• Mwanafunzi anakili kwenye daftari msamiati unaofunzwa. | 1) Je, unaweza kutambua vyakula vipi?<br>2) Ni chakula kipi unachokipenda?<br>3) Ni chakula kipi kinachofaidi mwili zaidi?<br>4) Ni chakula kipi kinachodhuru afya? |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vyakula vinavyofaa mwili ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>b) kuzungumzia juu ya chakula anachokipenda ili kuimarisha mazungumzo | • Mwanafunzi ataje baadhi ya vyakula kwa kuonyeshwa michoro na vyakula halisi.<br>• Wanafunzi wajadiliane kuhusu umuhimu wa vyakula mbalimbali k.m. vinavyompa mtu nguvu, vinavyomkinga mtu kutokana na magonjwa, vinavyoleta joto mwilini, vinavyowezesha mtu kukua n.k.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika mazungumzo kuhusu | 1) Unapenda kula chakula gani?<br>2) Chakula unachokila husaidiaje mwili?<br>3) Ni chakula kipi kinachoweza kudhuru afya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | c) kuzungumzia juu ya chakula kinachodhuru afya ili kuelewa madhara ya vyakula hivyo<br>d) kusikiliza masimulizi kuhusu lishe bora ili kujenga stadi ya kusikiliza<br>e) kuthamini vyakula vinavyofaidi mwili ili kuchagua vyakula kwa uangalifu. | chakula akipendacho.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika mjadala kuhusu chakula kinachodhuru afya k.m. vibanzi, biskuti<br>• Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa akisimulia kuhusu lishe bora na madhara ya vyakula vinavyodhuru afya<br>• Mwanafunzi aweza kuonyeshwa video kuhusu lishe bora na madhara ya vyakula hasi na baadaye washiriki katika mijadala ya vikundi. | kikiliwa sana? |
| | Kusoma: Hadithi (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kusikiliza hadithi ya mwalimu ili kuimarisha stadi za kusikiliza na kusoma<br>b) kusoma hadithi kwa mtiririko ufao ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>c) kufahamu hadithi aliyosoma na kusomewa ili kuelewa ujumbe katika hadithi<br>d) kuchangamkia kusoma hadithi ili kuendelea kujenga stadi ya kusoma. | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu anaposoma hadithi, asome pamoja na mwalimu kisha asome peke yake, wakiwa wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kupitia kinasasauti.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma na kusomewa hadithi.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video ya mtu au mtoto akisoma hadithi husika kwa ufasaha kisha aige usomi ule.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kuhusu hadithi.<br>• Mwanafunzi asimulie hadithi kutokana na picha alizopewa kuhusu lishe bora. | 1) Ni hadithi zipi ambayo umewahi kusoma?<br>2) Ni hadithi ipi iliyokufurahisha zaidi?<br>3) Unamkumbuka nani katika hadithi hiyo? |
| | Sarufi:Matumizi ya **hiki** na **hivi** | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: | • Mwanafunzi asome vifungu vinavyojumuisha **hiki** na **hivi** kama vile Kitabu hiki – Vitabu hivi; Kiti hiki – | 1) Unatumia neno gani kuonyeshea |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | (*Vipindi 2*) | a) kutambua matumizi ya **hiki** na **hivi** katika kuimarisha mawasiliano<br><br>b) kutumia **hiki** na **hivi** katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano<br>c) kusoma vifungu vinavyojumuisha **hiki** na **hivi** katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>d) kuandika vifungu vinavyojumuisha **hiki** na **hivi** katika kuimarisha stadi ya uandishi<br>e) kuchangamkia matumizi ya **hiki** na **hivi** katika mawasiliano. | Viti hivi; Kiatu hiki – Viatu hivi; Kifutio hiki – Vifutio hivi.<br><br>• Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwenye vifungu au sentensi zinazojumuisha **hiki** na **hivi**<br>• Mwanafunzi aonyeshe vitu mbalimbali kama vile vyakula ili kuvitungia sentensi katika vikundi k.m. chakula hiki – vyakula hivi.<br>• Mwanafunzi aweza kupewa vifungu vyenye mapengo wakamilishe kwa kutumia **hiki** na **hivi** wakiwa wawili wawili k.m. chakula __________ (hiki), vyakula __________(hivi). | ukaribu wa kitabu, kifutio, kiatu na kijiti?<br>2) Ni nini wingi wa **hiki**? |

| | |
|---|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>mawasiliano na ushirikiano – kujadili katika makundi au wawili wawili<br>hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi atajenga msingi wa kujua zaidi kuhusu lishe bora<br>ujuzi wa kidijitali –matumizi ya vifaa vya kiteknolojia. | |
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>elimu ya afya: magonjwa yanayohusiana na vyakula – kuthamini lishe bora | **Uhusiano na Maadili:**<br>uwajibikaji; mapenzi. |
| **Uhusiano na Masomo mengine:**<br>Health and Nutrition Activities na Environmental Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>kuwahamasisha wengine katika jamii kuhusu umuhimu wa lishe bora. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>kazi ya vikundi<br>michezo<br>vikundi vya ushirika shuleni. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kuuliza maswali kuhusu lishe bora<br>• kuchunguza jinsi anavyotumia msamiati katika sentensi<br>• kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa |

| | |
|---|---|
| | • kuchunguza jinsi anavyotumia hiki na hivi katika sentensi. |

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anatambua vyakula vinavyofaa na kuepuka vile vinavyodhuru<br>• anatumia msamiati wa lishe bora kwa ubunifu katika sentensi<br>• anasoma kwa ufasaha<br>• anafahamu kwa urahisi hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa.<br>• anatumia **hiki** na **hivi** katika sentensi kwa usahihi kila wakati<br>• anaandika kwa hati nadhifu na kwa haraka. | Mwanafunzi,<br>• anatambua vyakula vinavyofaa na vile vinavyodhuru<br>• anatumia msamiati wa lishe bora ifaavyo katika sentensi<br>• anasoma ifaavyo<br>• anafahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa<br>• anatumia **hiki** na **hivi** katika sentensi kwa usahihi<br>• anaandika kwa hati bora. | Mwanafunzi,<br>• anatambua vyakula vinavyofaa na vile vinavyodhuru<br>• ana changamoto za kutumia baadhi ya msamiati wa lishe bora katika sentensi<br>• anasoma baadhi ya kazi inazopewa<br>• anafahamu baadhi ya hadithi alizosimuliwa, aliyosoma au kusomewa<br>• ana changamoto katika kutumia **hiki** na **hivi** katika sentensi<br>• anaandika kwa hati zinazosomeka. | Mwanafunzi,<br>• ana changamoto katika kutambua vyakula vinavyofaa mwili na vile vinavyodhuru<br>• ana changamoto za kutumia msamiati wa lishe bora katika sentensi<br>• ana changamoto katika kusoma<br>• ana changamoto katika kufahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa<br>• ana changamoto katika kutumia **hiki** na **hivi** katika sentensi<br>• ana changamoto katika kuandika. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Mnyama Nimpendaye** | Msamiati<br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kuwatambua wanyama wa nyumbani kwa majina yao ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>b) kuelezea maana ya msamiati | • Mwanafunzi awatambue wanyama wa nyumbani kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo, ngamia na punda kwa majina yao kwa kutumia picha, michoro na wanyama halisi.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kutumia msamiati wa utunzaji wa wanyama kama vile lishe, | 1) Ni mnyama gani umpendaye?<br>2) Kwa nini unampenda mnyama huyo?<br>3) Unamtunzaje |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | unaotumiwa katika kutunza wanyama ili kuimarisha mawasiliano<br>c) kutumia majina ya wanyama katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano<br>d) kutumia msamiati unaohusu utunzaji wanyama katika sentensi ili kujenga mapenzi ya kuwatunza wanyama wa nyumbani<br>e) kuthamini umuhimu wa kuwatunza wanyama wa nyumbani. | zizi nk.<br>• Mwanafunzi aelezee msamiati unaotumiwa katika kutunza wanyama.<br>• Mwanafunzi achore baadhi ya wanyama na kuandika majina yao.<br>• Mwanafunzi aweza kuonyeshwa video ya utunzaji wa wanyama.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama michoro na picha za wanyama wa nyumbani na wanyama wakitunzwa. | mnyama umpendaye? |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kumtambua mnyama ampendaye ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>b) kusimulia kuhusu mnyama ampendaye ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>c) kusikiliza masimulizi kuhusu utunzaji wa wanyama ili kujenga usikivu<br>d) kuthamini wanyama ili kushiriki katika kuwatunza. | • Mwanafunzi atambue mnyama ampendaye kupitia kwa maswali na majibu.<br>• Mwanafunzi asimulie kuhusu mnyama ampendaye katika darasa, wakiwa wawili wawili na katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusimuliwa jinsi ya kutunza wanyama kupitia kwa mgeni mwalikwa.<br>• Mwanafunzi aweza kuwatambua wanyama wa nyumbani kwa kutumia michoro na picha halisi.<br>• Mwanafunzi aweza kuonyeshwa video inayohusu utunzaji wa wanyama mbalimbali.<br>• Wanafunzi waweza kushiriki katika mjadala kuhusu jinsi wanavyowatunza wanyama wawapendao. | 1) Ni mnyama gani umpendaye?<br>2) Kwa nini unampenda mnyama huyo?<br>3) Unamtunzaje mnyama umpendaye? |
| | Kusoma: Hadithi | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi. | 1) Umewahi kusoma hadithi kuhusu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | (*Vipindi 4*) | a) kusikiliza hadithi ya mwalimu ili kujenga usikivu<br>b) kusoma hadithi kwa mtiririko ufao ili kuimarisha usomaji<br>c) kufahamu hadithi aliyosoma na kusomewa ili kuelewa ujumbe<br>d) kupenda kusoma hadithi kuhusu wanyama wa nyumbani ili kuendeleza usomaji. | • Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br><br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu anaposoma hadithi, asome pamoja na mwalimu kisha asome peke yake, wakiwa wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kupitia kinasa sauti.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma na kusomewa hadithi.<br>• Mwanafunzi aweza kutazama video ya mtu au mtoto akisoma hadithi husika kwa ufasaha kisha aige usomi ule.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kuhusu hadithi aliyosoma na kusomewa.<br>• Mwanafunzi aweza kusimulia hadithi kutokana na picha alizopewa kuhusu wanyama wa nyumbani. | wanyama gani wa nyumbani?<br>2) Unakumbuka nini katika hadithi hiyo? |
| | Sarufi:<br>Matumizi ya **Hili** na **Haya**<br>(*Vipindi 2*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua matumizi ya **hili** na **haya** ili kuimarisha mawasiliano<br>b) kutumia **hili** na **haya** katika sentensi sahihi ili kuimarisha mawasiliano<br>c) kusoma vifungu vinavyojumuisha matumizi ya **hili** na **haya** ili kujenga usomaji<br>d) kuandika vifungu | • Mwanafunzi asome vifungu vyenye matumizi ya **hili** na **haya** kama vile embe hili – maembe haya; dawati hili – madawati haya; jani hili – majani haya.<br>• Wanafunzi waweza kujaza mapengo kwa kutumia **hili** na **haya**.<br>• Mwanafunzi aonyeshwe vitu mbalimbali kama vile tunda kwa kurejelea **hili** na **haya** kwa mfano: tunda hili – matunda haya; embe hili – maembe haya n.k.<br>• Mwanafunzi aweza kukamilisha mafungu yanayohusu matumizi ya **hili** na **haya** wakiwa | 1) Unatumia neno gani kuonyeshea tunda lililo karibu nawe?<br>2) Unatumia neno gani kuonyeshea dawati lako? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | vinavyojumuisha matumizi ya **hili** na **haya** ili kuimarisha uandishi bora<br><br>e) kuchangamkia matumizi ya **hili** na **haya** katika mawasiliano. | wawili wawili k.m. tunda __________ (hili), matunda __________(haya).<br>• Mwanafunzi aweza kufanya mazoezi mbalimbali katika tarakilishi kuhusu mada. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
mawisiliano na ushirikiano - wanafunzi washiriki katika vikundi na wakiwa wawili wawili
ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza hadithi msamiati na sauti
kufikiri kwa kina – kung'amua sifa za mnyama ampendaye.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>Elimu ya maendeleo endelevu: masilahi ya wanyama – kujali na kutunza mnyama. | **Uhusiano na Maadili:**<br>mapenzi kwa wanyama. |
| **Uhusiano na masomo mengine:** Environmental activities, English activitites. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>kuwahamasisha wanajamii kuhusu utunzaji wa wanyama. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>kushiriki katika vikundi vya ushirika wa wanafunzi. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kuuliza maswali kuhusu wanyama<br>• kuchunguza jinsi anavyotumia msamiati wa wanyama katika sentensi<br>• kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa<br>• kuchunguza jinsi anavyotumia **hili** na **haya** katika sentensi<br>• kufuatilia jinsi anavyoandika na kuchora. |

**Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|
| Mwanafunzi,<br>• anatambua wanyama wa nyumbani kwa majina na kuyatumia kuwataja kila wakati | Mwanafunzi,<br>• anatambua wanyama wa nyumbani kwa majina yao<br>• anasimulia visa na matukio | Mwanafunzi,<br>• anatambua wanyama wa nyumbani kwa majina yao<br>• anasimulia visa na matukio | Mwanafunzi,<br>• anatambua baadhi ya wanyama wa nyumbani kwa majina yao<br>• ana changamoto katika kusimulia |

| | | | |
|---|---|---|---|
| • anasimulia visa na matukio kuhusu wanyama kwa ubunifu na ufasaha<br><br>• anatumia msamiati wa wanyama kwa ubunifu katika sentensi<br>• anasoma kwa ufasaha.<br>• anafahamu kwa urahisi hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa<br>• anatumia **hili** na **haya** katika sentensi kwa usahihi kila wakati<br>• anaandika maneno na sentensi kwa hati nadhifu na kwa haraka. | kuhusu wanyama kwa ufasaha.<br>• anatumia msamiati wa wanyama ifaavyo katika sentensi<br>• anasoma ifaavyo<br>• anafahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa.<br>• anatumia **hili** na **haya** katika sentensi kwa usahihi.<br>• anaandika maneno na sentensi kwa hati bora. | kuhusu wanyama<br>• anatumiabaadhi ya msamiati wa wanyama ifaavyo katika sentensi<br>• anasoma baadhi ya maneno na sentensi<br>• anafahamu baadhi ya hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa<br>• anatumia **hili** na **haya** katika baadhi ya sentensi kwa usahihi<br>• anaandika maneno na sentensi kwa hati zinazosomeka. | visa na matukio kuhusu wanyama<br>• ana changamoto katika kutumia msamiati wa wanyama ifaavyo katika sentensi<br>• ana changamoto katika kusoma<br>• ana changamoto katika kufahamu hadithi aliyosimuliwa, aliyosoma na kusomewa<br>• ana changamoto katika kutumia **hili** na **haya** katika sentensi kwa usahihi<br>• ana changamoto katika kuandika. |